**Learning By Ear 2011 Biashara – Kuanzisha Biashara**
**Kipindi cha 2: "Biashara ni nini?"**
AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel, Adrian Kriesch
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

## Characters

Msimulizi

Daniel Huba (Mwanamume, umri wa miaka 29, Mwingereza)

**Scene 1:**

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka 18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka 19)

**Scene 2:**

**KOSSI:** (Mwanamume, umri wa miaka 18)

**ABBAS:** (Mwanamume, umri wa miaka 21)

**MARIAM:** (Mwanamke, umri wa miaka 19)

**INTRO**

**Host:**

Hujambo na karibu kwenye Noa Bongo Jenga Maisha Yako, kipindi cha pili cha mfululizo wa vipindi vyetu kuhusu jinsi ya kuanzisha biashara. Rafiki zetu watatu, Mariam, Abbas na Kossi, wamedhamiria kuanzisha kampuni yao wenyewe. Wameibuka na fikira ya kipekee. Bwana Masinga, mjasiriamali aliyebobea, aliye na ukuruba na familia ya kina Mariam, amejitolea kuwasaidia. Mada ya kipindi cha leo ni “Biashara gani?”, na kinaanza na

ushauri wa Daniel Huba, mhadhiri katika Kituo cha Ustawi wa Ujasiriamali, Chuo Kikuu cha Inoorero nchini Kenya.

**1. Daniel Huba: 38''**

*Naam, tukumbuke mara iliyopita tulisema jambo la kwanza ni kuwa na wazo la biashara. Je, wazo kama hilo hutoka wapi? Linaweza kutokea vivi hivi, kutokana na tajriba ya mtu. Mtu anaweza kukisia jambo fulani akasema: Ninataka kufanya hivyo. Wanaweza pia kupata wazo kwa kuzungumza na watu, marafiki au wenzao. Wazo pia linaweza kuzuka mtu anapotambua mahitaji ya watu. Unaweza kwenda kijijini au mjini kwenu ukawauliza watu vitu wasivyo navyo. Wangetaka nini na nini ninachoweza kuwaletea?*

**2. Narrator:**

Marafiki zetu watatu wanapaswa kujiuliza swali hili. Je wataendelea na mpango wao, au watafuata njia nyingine? Ebu tumsikilize Abbas, anayemsubiri mchumba wake Mariam na Kossi rafiki yake.

**<u>Scene 1: At Abbas'</u>**

**KOSSI, ABBAS, MARIAM**

**3. SFX : Inside atmo, in the living room. Radio in the background.**
**4. SFX : Things being put away…**

**5. ABBAS:** (**Sighs deeply**) Ni karibu saa kumi tayari. Kwani Mariam ana nini? Kossi atafika wakati wowote kuanzia sasa… Naam, nitampigia simu Mariam.

| | |
|---|---|
| **6. SFX: Number being dialed on a mobile phone** | |

7. **ABBAS:** Hallo? Mariam! Hallo! Uko wapi? Ungali nyumbani? Inakaribia saa kumi na  Kossi yuko karibu kufika. Nini? Fanya haraka. Unamjua kwamba si mtu wa kuchelewa!

| |
|---|
| **8. SFX: Sound of a mobile being switched off** |
| **9. SFX: motorbike arrives outside** |

10. **ABBAS:** Salala, isiwe kwamba ameshafika tayari…. Pengine…

| |
|---|
| **11. SFX: Door opens and steps approach** |

12. **KOSSI:** (**Whistling happily**) Hujambo, rafiki yangu. Upo? Mambo vipi?

13. **ABBAS:** Nipo kama kawaida tayari kukufaa kwa vyovyote.

| |
|---|
| **14. Atmo: African-style hand and finger snapping as greeting** |

15. **KOSSI:** Eee … mchumba wako yu wapi?

16. **ABBAS:** Ameshataka radhi, atachelewa kufika.

**17. KOSSI:** Naam, tulisema nini vile? Kwamba tutazingatia wazo langu, natumaini!

**18. ABBAS:** Tulia! Tulisema tutashauriana na jamaa na marafiki zetu kupata mawazo. Tumsubiri Mariam kisha tulizungumzie suala hilo!

**19. KOSSI:** Ebu, usiniambie kwamba nyinyi wawili hamjalizungumzia suala hili.

**20. ABBAS:** (**annoyed**) Hatujalizungumzia. Mimi na yeye, kila mtu na mawazo yake.

**21. KOSSI:** (**Bursts out laughing**) Aha haa, mambo ya uchumba wa kisasa hayo!

**22. SFX: Sound of steps (woman) running, door opens**

**23. MARIAM:** (**Bursts in, out of breath**) Hamjambo, samahani… HAYA, tunaweza kuanza. (**Silence**). Haraka haraka tupitie mawazo na mapendekezo yote tuliyopata, kisha tutaamua!

**24. ABBAS:** Nilishauriana na marafiki wachache na binamu yangu. Mawazo yao hayakunipendeza kusema kweli. Walinishawishi tuingilie mradi hatari. Ila binamu yangu- alipendekeza tuanzishe afisi ya kuwapa

ushauri wa kisheria akina mama walioko sokoni. Wengi wao hawajasoma na hawajui jinsi ya kutetea haki zao.

**25. KOSSI:** Hilo si wazo baya. Lakini tunapaswa kuwa na uzoefu wa masuala ya kisheria ambao hatuna! Mhadhiri wangu wa masuala ya masoko alipendekeza tuanzishe kampuni ya habari au tutoe huduma za ushauri katika nyanja ya mawasiliano. Shughuli hiyo siku hizi ndiyo iliyo na faida kubwa.

**26. MARIAM:** Ati? Lakini tayari kampuni hizo zimejaa kila pahali, hilo si wazo la kipekee… Baadhi ya watu niliozungumza nao wanasema tuanzishe kituo cha kutibu ng'ombe au biashara ya kilimo, kama vile shamba. Walisema tuna ardhi kubwa sana hapa na pia watu wengi waliosomea somo la kilimo, na kwamba kazi hiyo itatusaidia pia kujitegemea kwa chakula.

**27. KOSSI:** Naona mada hii inaafiki kwa kuwa tayari wawili wetu wanaichangamkia. Mimi tangu hapo nilitaka kuwa mtaalamu wa uchumi wa kilimo naye Mariam alitaka kusomea tiba ya wanyama.

**28. MARIAM:** Sijakata tama bado… Naomba niendelee kidogo: kulikuwa pia na wazo la kuanzisha mkahawa mdogo, na wazo lenyewe halikuwa tafauti na wazo langu

kuhusu baa. Kuuza chakula na vinywaji katika jiji ambalo linakua kwa kasi.

**29. ABBAS:** Si wazo baya. Rafiki yetu Kutino alipendekeza tuanzishe kampuni ya usanifu. Na marafiki zangu wacheza kamari walisema tunaweza kuanzisha taasisi ya kifedha ya kufadhili biashara ndogo ndogo kuwasaidia watu maskini. Na kuna watu wengi maskini hapa.

**30. KOSSI:** (**Bursts out laughing**) Hilo ni wazo la kuchekesha. Tufuateni nyayo za yule raia wa Bangladeshi aliyeshinda tuzo ya Noble kwa sababu ya benki yake ya kusaidia watu masikini …

| **31. SFX Mobile phone rings** |
|---|

**32. KOSSI**: Samahani! Subirini kidogo… **(answers**) Hallo? …HAYA. **(Puts down the phone. Speaks to his friends)** Ni mamangu. Acheni niondoke. Kuna dharura.

| **33. SFX: Chair being pulled back**. |
|---|

**34. ABBAS:** SAWA. Bora tukutane kesho kutwa papa hapa na wakati kama huu.

**35. MARIAM:** Huenda tutakuwa na mawazo mengine mapya machache.

**36. SFX: Door opens**

**37. KOSSI:** (**From a distance**) HAYA, kwaherini!

**38. Narrator:** Kama ulivyosikia, wenzetu wana mawazo mengi. Lakini wafanye nini? Tusikie ushauri kutoka kwa mtaalamu wetu Daniel:

**39. Daniel Huba: 38''**

*Njia bora ya kutekeleza mpango mzuri wa biashara ni kuandika mawazo yako. Haina maana kwamba uandae mpango wa kina, lakini unaweza kusema kwa mfano "Ningependa kuuza mboga". Kwa hivyo hatua ya mwanzo ya kuandika mpango wako inakufanya ujiulize ' Haya, ninahitaji kufanya nini ili kutekeleza biashara hii?' Ninapaswa kuzungumza na kina nani ninapotaka kufanya biashara hii? Unaandika taarifa hiyo kisha unaanza kuangalia jinsi wazo hilo la biashara linavyoweza kuwianishwa na mahitaji ya soko unalolenga.*

## Scene 2: At ABBAS's

**KOSSI, ABBAS, MARIAM**

| |
|---|
| **40. SFX : Inside, music/radio in the background** |

| | |
|---|---|
| **41. KOSSI:** | (**Silence**) Sawa, sikizeni. Nadhani tuna mawazo mengi sana sasa. Iwapo hatutazingatia mawazo bora zaidi huenda tukakosa mwelekeo. |
| **42. MARIAM:** | Lakini sijawaambia mawazo mapya ambayo nimepata! |
| **43. ABBAS:** | Acha tuyasikie. |
| **44. KOSSI:** | (**Exasperated**) Mawazo zaidi? |
| **45. ABBAS:** | Hakuna shida tukiyasikia. Haya, Mariam twambie. |
| **46. MARIAM:** | Marafiki zangu wa kike wanasema tuanzishe kiwanda kidogo cha kutengeneza vipodozi kutokana na mimea ya kienyeji. Nao marafiki zangu wa chama cha wanafunzi wa zamani wanapendekeza tuanzishe mradi wa mfumo wa mtandao, kwa kimombo, Coalition for a Well-Made Africa, yaani CWMA. Aina fulani ya taasisi ya kuteua na kuwafunza watu kufanya kazi katika sekta ya jua kali, sekta ambayo ndiyo kubwa zaidi barani Afrika. |

**47. KOSSI:** (**Happy**) Sawa, lakini sikizeni – mawazo yamezidi sasa. Tutachanganyikiwa. Hatutamakinika tukiendelea hivi. Ninapendekeza tuchague mawazo mawili au manne ya kipekee kisha tuyaandike.

**48. MARIAM:** Kwa nini tuyaandike?

**49. KOSSI:** Ili tuweze kudhibiti mawazo yetu. Tujue tunakoelekea na tuweze kutoa maamuzi upesi. Vinginevyo tutapoteza muda mwingi, SAWA?

**50. ABBAS and MARIAM:** (**In chorus**) SAWA!

**51. KOSSI:** (**to MARIAM**) Mariam, ebu rejelea tuliyoyasema – Abbas, nawe uandike!

**52. MARIAM:** HAYA! Kumbukeni alivyotwambia Bwana Masinga – tunahitaji mawazo ya kipekee … Kulingana na yote tuliyoyataja, nadhani afisi ya kutoa ushauri wa kisheria kwa kina mama sokoni ni wazo zuri.

**53. ABBAS:** Nadhani ni wazo la kipekee, na tayari kuna kundi kubwa linalolengwa. Unahitajika utaalamu wa kisheria, na kwa hivyo mambo yako wazi hatuna cha kutapatapa kutafuta rai kwengine …

**54. KOSSI:** (**Agrees**) SAWA. Nini tena?

**55. MARIAM:** Shughuli ya ukulima na ufugaji?

**56. KOSSI:** (**Lively**) Naam, hiyo inahitajika sana. Ni shughuli inayohusu jamii, pia, na tunaifahamu shughuli yenyewe..

**57. MARIAM:** (**Peremptorily**) Wazo la duka la nguo halijanivutia, na tena tayari kuna maduka mengi sana ya nguo

**58. KOSSI:** Vivyo hivyo kuhusu mkahawa au baa - zimetapakaa kila mahali…

**59. MARIAM:** Na vipi kuhusu wazo la kuanzisha benki ya masikini?

**60. ABBAS:** (**Jumps on it**) Naam, ni wazo la kipekee. Benki itakayowakopesha fedha watu masikini zaidi, kwa viwango vya chini sana vya riba na bila kuhitaji dhamana kubwa kubwa – mradi huo ungewanufaisha sana watu wengi. (**Silence**) Nilipendekeza pia kuhusu kampuni ya usanifu. Hapa hatuna kampuni nyingi za aina hiyo ingawa huduma zake zinatakikana sana. Sote tunajua vizuri mambo ya mtandao na tunaweza kujifunza habari za usanifu upesi. Tunatakiwa tu tuelemee uwanja maalum wa usanifu.

**61. KOSSI:** Naam, hilo pia si wazo baya …

AUTHOR: Erick-Hector HOUNKPE
EDITORS: Yann Durand, Aude Gensbittel, Adrian Kriesch
TRANSLATOR: Anne Thomas
PROOFREADER: Charlotte Collins

**62. ABBAS:** (**Interrupts him**) SAWA, ebu tuyapitie yale ambayo nimeandika. Kwanza – ushauri wa kisheria; pili, kilimo na ufugaji; tatu, benki ya watu maskini; na nne, kampuni ya usanifu …. (**Silence**)

**63. KOSSI:** **(catches a breath)** Bado hatujamakinika!

**64. ABBAS:** Ndiyo, lakini sasa orodha ni fupi na inaeleweka zaidi.

**65. MARIAM:** **(Continues**) Na tukiwa na orodha hii tutaweza kufikiria tena kuhusu haya mawazo yetu na kuyachanganua vilivyo ili tufanye maamuzi yanayofaa.

**66. KOSSI:** (**Still confused)** Lililobaki sasa ni kuchagua.

**67. ABBAS:** Naam, lakini si hayo tu. Tukishachagua wazo, itatubidi tulitathmini, tuchunguze soko, gharama, rasilimali na jinsi ya kuzifanyisha kazi ….

**68. KOSSI AND MARIAM:** (**Burst out laughing**)

**69. MARIAM:** Naam, umesema kweli! Tunatakikana kufanya haraka!

**70. Narrator:** Wenzetu watatu wanakabiliwa na kibarua kigumu. Lakini jambo moja ni dhahiri– kwamba wana moyo. Na hilo ni jambo muhimu, kama anavyosema mtaalamu wetu Daniel.

**71. Daniel Huba: 38''**

*Huenda mtu ukawa na mawazo mazito ya kipekee, ambayo hayajatendeka hapo awali. Unapojaliwa kuwa na mawazo sampuli hiyo, bahati yako! Lakini iwapo hutajaliwa kuwa na mawazo ya kipekee usikate tama. Watu hujifunza kutokana na wenzao. Mjasiriamali anapaswa kujitahidi kutimiza mahitaji ya soko lakini si lazima mahitaji hayo yawe mapya. Pengine biashara fulani zipo sokoni lakini si nyingi kuweza kutoa huduma au bidhaa zinazohitajika. Mwongozo wako unapaswa kuwa "Je kuna soko la kitu ulichonuia kufanya?" Ikiwa soko lipo, basi tekeleza wazo lako mara moja!*

**OUTRO**

**Host:**

Hicho kilikuwa kipindi cha pili cha mfululizo wa vipindi vyetu vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako kuhusu kuanzisha biashara, vinavyomshirikisha mtaalamu Daniel Huba wa Chuo Kikuu cha Inoorero mjini Nairobi. Je Kossi, Abbas na Mariam watazingatia wazo gani? Kwa taarifa zaidi usikose kukisikiliza kipindi kifuatacho. Je umewahi kufikiria kuanzisha biashara yako binafsi? Je umeshafanya hivyo? Tuandikie utufahamishe mawazo na uzoefu wako kuhusiana na masuala haya kwa barua-pepe: lbe@dw-world.de

Ikiwa ungependa kusikiliza tena kipindi hiki au vipindi vingine vya Noa Bongo Jenga Maisha Yako, tembelea wavuti yetu www.dw.de/kiswahili.

Usikose kututegea sikio katika kipindi kinachofuata! Kwaheri!

**END**